# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.

## OFISI YA RAIS,

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA MERU


**SHULE YA SEKONDARI PAMOJANGABOBO,**

**S.L.P 102,**

**USA RIVER.**


**Kumb. Na. PSS/CG/Vol.1**


**+255 757 270 772 MKUU WA SHULE**
**+255 624 046 774 au +255 768 510 175 MAKAMU MKUU WA SHULE**


**Ndg. Mzazi wa ………………………………………………………………………………………**

**YAH: <u>MAAGIZO KWA WAZAZI WA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2025</u>**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao ………………………………………………………… amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2025 katika shule hii. Hongera sana! **Tafadhali hakikisha kuwa mwanao hatakosa kufika shuleni siku ya kufungua shule**. Ni muhimu mwanao kufika shuleni siku hiyo ili aweze kushiriki kikamilifu katika ratiba iliyoandaliwa ya masomo.

**MAAGIZO YA MAHITAJI**

**1. SARE YA SHULE**

**a) Mvulana**

Aje na:

i. Suruali mbili za rangi nyekundu (gredi 1, zisiwe za kubana na ziwe na selebresheni mbili. Upana wa suruali kwa chini uwe wa saizi ya sentimeta 16.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi mapya, na mashati hayo yatapigwa nembo ya shule hapa shuleni.
iii. Sweta mbili nyekundu
iv. Tai ndefu nyekundu mbili zenye mistari meupe
v. Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba na viwe vya ngozi
vi. Soksi nyeusi jozi mbili au zaidi.

vii. Suruali mbili za rangi nyekundu za kushindia isiyobana yenye selebresheni na mstari mweupe kutoka kiunoni hadi chini kwa miguu yote miwili.
viii. Tishet mbili nyekundu zisizo na kola.
ix. Nguo za michezo: bukta mbili nyekundu zenye mistari meupe na tisheti nyekundu yenye mistari meupe pamoja na viatu vya michezo na soksi ndefu za rangi nyekundu.
x. Traki suti nyekundu yenye mistari meupe
xi. Taulo ya kutumia baada ya kuoga.
xii. Shuka mbili za bluu bahari na blanketi moja

**b) Msichana**

Aje na:

i. Sketi mbili nyekundu (gredi 1, mashono ya solo) ndefu kufikia kifundo cha mguu
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi mapya. Mashati hayo yatapigwa nembo ya shule hapa shuleni.
iii. Sweta nyekundu mbili
iv. Tai ndefu nyekundu mbili zenye mistari meupe (zinapatikana madukani)
v. Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba na viwe vya Ngozi
vi. Soksi nyeupe jozi mbili au zaidi
vii. "Shamba dress" mbili: sketi mbili nyekundu zenye marinda ndefu kufikia kifundo cha mguu na tisheti mbili nyekundu zisizo na kola.
viii. Nguo za michezo: bukta mbili nyekundu zenye mistari meupe na tisheti nyekudu yenye mistari meupe pamoja na viatu vya michezo na soksi ndefu za rangi nyekundu.
ix. Tisheti mbili nyekundu zisizo na kola
x. Traki suti nyekundu yenye mistari meupe
xi. Taulo ya kutumia baada kuoga
xii. Shuka mbili za pinki na blanket moja

## 2. VIFAA VYA DARASANI

i. Madaftari makubwa (Counter books) yasiyopungua 12,
ii. "Mathematical set"
iii. Kalamu za wino na penseli za kutosha
iv. Mkoba imara wa kubebea madaftari
v. Vitabu vya kusoma kwa masomo yote kidato cha kwanza.
vi. Rimu mbili za karatasi (1 nyeupe na 1ya mistari )

## 3. VIFA VYA USAFI WA NJE

i. Soft broom moja. ***(kwa wasichana)***
ii. Fagio ya chelewa moja ***(wote)***
iii. Mkasi mkubwa kwa ajili ya kuchonga maua na fensi (***kwa wavulana***)
iv. ...............................................................................................................

## MAHITAJI YA HOSTEL

i. Godoro (2.5ft upana na 6ft urefu)
ii. Tochi moja kwa ajili ya dharura pale mwanga unapokosekana
iii. Net ya mbu
iv. Ndoo ya kuhifadhia maji ya kunywa (2)
v. Sanduku la bati (tranker)
vi. Vifaa vya usafi binafsi kama sabuni ya kuogea na kufulia, mafuta ya kupaka, kiwi, kitana, malapa, mswaki na dawa ya meno.
vii. Vyombo vya chakula (sahani ya aluminum 1, kikombe cha nusu lita cha aluminium 1 na kijiko 1)

## A. MAELEKEZO KWA WAZAZI

Sheria mama za shule zimebainishwa katika kiambatisho B. Wazazi na mwanafunzi/wanafunzi ni muhimu kusoma kwa uangalifu na kutia saini zenu katika sehemu ya makubaliano katika kiambatisho hicho. Halafu **mzirudishe kwa mkuu wa shule**. Ni dhahiri kuwa wanafunzi watakuwa wanapoteza wakati wao bure kama wasipotaka kufanya kazi zote kwa bidii na kutii sheria za shule.

## B. FOMU YA UCHUNGUZI WA KIAFYA

Hakikisha mwanao amepimwa na daktari na kujaza taarifa kwenye ***"medical examination form"*** ambayo iko katika fomu kiambatisho A.

## C. SHERIA ZA SHULE

Pamoja na barua hii, nimeambatanisha makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule.

## D. HITIMISHO

Wazazi tunaomba sana tuwe na malezi ya pamoja ili watoto wetu wakue katika maadili mema na kuwawezesha kupata kile walichokifuata hapa shuleni Pamoja, yaani **ELIMU.** Msisitizo ni kwamba kila mwanafunzi anatakiwa kusoma kwa bidii na kufaulu kwa kiwango cha ***alama 65*** au zaidi katika kila somo. Sheria zote za shule zinalenga katika kumfanya mtoto apate mazingira bora ya kujisomea na hatimaye aweze kufaulu vizuri masomo yake.

TUNATEGEMEA SANA USHIRIKIANO WAKO

………………
JOHN P. AWE
MKUU WA SHULE.

## TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI.

**PICHA YA MWANAFUNZI**

Mimi {taja majina matatu} ……………………………………………………… {Jinsi}………., umri wangu ni miaka ………………
Jina la baba …………………………………kazi yake………………………namba ya simu ya baba ………………..
Jina la mama ………………………………..kazi yake……………………… namba ya simu ya mama………………………
Ninaishi kijiji cha ………………………………… kata ya ……………………………wilaya ya…………………………… mkoa wa ……………………………… namba ya afisa mtendaji wa kijiji changu………………………………………

Je una wazazi wote? ***(weka alama ya v panapohusika).***
Wawili { } mmoja { } hapana { }

Kama una mzazi mmoja ni ***(weka alama ya v panapohusika).***
Baba { } au ni mama { }

Saini ya mwanafunzi…………………………………………….

## TAARIFA BINAFSI ZA MZAZI/MLEZI.

**PICHA YA MZAZI/MLEZI**

Mimi (majina matatu)………………………………………………………... mzazi/mlezi wa……………………………………… Ninaahidi kumtimizia mwanangu mahitaji yake yanayostahili wakati atakapokuwa shuleni.

Nitashirikiana na uongozi wa shule pindi nitakapohitajika shuleni. Pia kama nitakosekana nitawakilishwa na ………………………………………ambaye ni ………………………………………………..wa mwanafunzi mtajwa hapo juu.

Saini ya mzazi/mlezi…………………………………

Saini ya mkuu wa shule……………………………..

**THE PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**PAMOJANGABOBO SECONDARY SCHOOL MEDICAL**

**EXAMINATION FORM**

To be completed by medical officer in any government hospital of all new entrance to Pamojangabobo secondary school.

Full name of the student……………………………………………………………………

Age………………………… sex…………………………….

1. Blood count (red and white) blood cells…………………………….
2. Urine examination…………………………………………….
3. Stool examination…………………………………………………..
4. Syphilis test…………………………………………………….
5. TB test……………………………………………………………………..
6. Ear test………………………………………………………………………
7. Eye test……………………………………………………………………………..
8. Spleen ………………………………………………………………………..
9. Abdomen …………………………………………………………………….
10. Additional information or any other physical, mental, heredity or infectious diseases ………………………………………………………………………………………………… ………………………………..

Treatment after examination……………………………………………………………………………………….

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above mentioned has been examined and found fit/not fit to pursue secondary education

Name:…………………………………………………….. Signature:…………………
Date:……………………………

Station:……………………………………………. Designation:……………………………..

Official stamp:…………………………………………………

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI PAMOJANGABOBO**
**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Mwanafunzi anayejiunga katika shule hii anapaswa kuzisoma vizuri sharia na kanuni za shule kisha atasaini Pamoja na mzazi au mlezi wake wakati wa kuripoti na atarudisha hati hii shuleni.

Mwanafunzi awapo shuleni anapaswa kuzingatia yafuatayo:

1. Kuishi na kutenda kulingana na maadili ya uanafunzi.
2. Heshima miongoni mwa wanafunzi na kuwaheshimu walimu, walezi na jumuiya nzima inayoinzunguka shule.
3. Kuvaa sare ya shule wakati wote wa masomo na nyakati zingine utakapohitajika kufanya hivyo.
4. Ruhusa zote za kutoka nje ya mipaka ya shule zinatolewa na ofisi ya malezi au mwalimu wa zamu.
5. Ni marufuku mwanafunzi kutembelea nyumba za wafanyakazi wa shule bila idhini maalumu kutoka katika ofisi ya malezi na nidhamu.
6. Ni marufuku mwanafunzi kuwatembelea wanafunzi wa jinsia tofauti na yeye wakati wakiwa kwenye mabweni yao.
7. Wanafunzi wote wanapaswa kuishi kama ndugu au kama kaka na dada kwa hiyo ni kosa kwa mwanafunzi kuonesha kwa namna yoyote kuwa wanaisha kama mtu na mpenzi wake.
8. Mgeni atayekutembelea sharti apate kibali kutoka katika uongozi wa shule. Ni marufuku kumtembeza mgeni yeyote katika maeneo ya shule bila kibali cha uongozi wa shule.
9. Ni marufuku mwanafunzi yeyote kuwa na nywele zisizopunguzwa na kutunzwa vizuri, kunyoa kipara, kufuga ndevu na sharafa, kuacha kucha ndefu na kuvaa mavazi kama vile koti, jaketi, sketi fupi/iliyofupishwa, kupaka kucha rangi, kutinda nyusi, rasta, lipstick/shine na mapambo yasiyoruhusiwa.
10. Ni marufuku mwanafunzi kuchora au kuandika kwenye kuta, meza madawati, viti vya kukalia, milango au sehemu nyingine yeyote ambayo hairuhusiwi.

**MAKOSA YAFUATAYO YATASABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi wa aina yoyote.
2. Uvutaji wa bangi, sigara na madawa ya kulevya.
3. Kupigana, kupiga au kuchochea ugomvi.
4. Kuharibu mali ya umma kwa makusudi.
5. Kudharau bendera ya taifa au wimbo wa taifa.
6. Kuoa au kuolewa.
7. Kumpa msichana mimba au au kupewa mimba, kutoa mimba au kusaidia kutoa mimba.
8. Kuwa mtoro vipindi vya darasani.

9. Kuonekana kwenye nyumba za starehe mfano nyumba ya kulala wageni, bar au mabanda ya kuangalia mpira au sinema.
10. Kuwa na simu ya mkononi au laini au kifaa chochote cha umeme kisichoruhusiwa.
11. Kuwa na pasi ya umeme au ya mkaa, jiko na vifaa vingine vinavyoweza kusababisha ajali ya moto.

NB: kama una tatizo lolote, mawasiliano yafanyike kupitia uongozi wa wanafunzi, mwalimu wa zamu, walimu wa madarasa, walezi wa mabweni au uongozi wa shule ili kuepusha migogoro shuleni.

Mimi………………………………………………………………. Nakubali kutii sheria na maagizo haya ya shule. Pindi nitakapovunja sheria na maagizo haya, hatua kali zichukuliwe kulingana na sheria na taratibu za shule.

Jina la mzazi/mlezi………………………………saini…………………tarehe…………